TANGAZO LA SERIKALI NA. 926 la tarehe 15/11/2024

SHERIA YA MADINI,
(SURA YA 123)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 27C(5))*

NOTISI YA RUHUSA YA KUTOFANYA BIASHARA YA MADINI MAALUM KATIKA MASOKO YA MADINI NA VITO

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Ruhusa ya Kutofanya Biashara ya Madini Maalum katika Masoko ya Madini na Vito ya Mwaka 2024.

Ruhusa ya madini maalum

2.-(1) Madini yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii yanapewa ruhusa ya kutokuuzwa katika Masoko ya Madini na Vito.

(2) Bila kuathiri aya ndogo ya (1), Tume itaanzisha vituo vya ununuzi vinavyohamishika na visivyohamishika vilivyotengwa karibu na maeneo yenye shughuli za uchimbaji madini kuhusiana na madini yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii.

Sura ya 123
TS. Na. 418 la 2019

(3) Vituo vya ununuzi vinavyotembea na visivyohamishika vilivyorejewa chini ya aya ndogo ya (2) vitachukuliwa kuwa na hadhi sawa na Masoko ya Madini na Vito yaliyoanzishwa chini ya Sheria ya Madini na Kanuni za Masoko ya Madini na Vito ya Mwaka 2019.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2(1))*

| Na. | Aina ya Madini | Maelezo |
|---|---|---|
| 1. | Madini ya Viwanda | Chokaa, Chumvi, Madini ya Udongo wa Mfinyanzi, Silika, Ulanga |
| 2. | Madini ya Nishati isipokuwa Madini Nururishi | Makaa ya mawe |
| 3. | Vito vya Daraja la Biashara na Viwanda | Feldspar, Ganeti, Kwati, Corundum |
| 4. | Madini ya Ujenzi | Mchanga, Changarawe, Vigae, Matale, Marumaru, Basalt, Fuwawe |
| 5. | Madini yasiyo na Metali | Mawe yenye madini ya Chuma, Mawe yenye madini ya Shaba Nyekundu, Boksiti, Mawe yenye madini ya Nikeli, Miamba iliyo na Risasi, Kromite |

Dodoma
8 Novemba, 2024

ANTHONY PETER MAVUNDE
*Waziri wa Madini*